

جمهورية تنزانيا الاتحادية  
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
وزارة التربية والتعليم والعلوم والتكنولوجيا  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



مقرر اللغة العربية للمرحلة الابتدائية  
MUHTASARI WA LUGHA YA KIARABU  
ELIMU YA MSINGI  
الصف III - VI  
DARASA LA III-VI  
2023

© مؤسسة تنزانيا للتربية، 2023م  
الطبعة الأولى 2023م

رقم ISBN 978-9987-09-835-4

مُؤَسَّسَةُ تَنْزَانِيَا لِلتَّرْبِيَّةِ  
132 شَارِع، عَلِيّ حَسَنٌ مُؤَيَّنِي  
مَكُونِيْن A  
ص.ب 35094  
14442 دَارُ السَّلَام

رَقْمُ الْهَاتِفِ: +255 735 041 170 / +255 735 041 168  
الْبَرِيدُ الْإِلِكْتُرُونِيُّ: director.general@tie.go.tz  
المَوْقِعُ الْإِلِكْتُرُونِيُّ: www.tie.go.tz

ينبغي توثيق هذا المقرر على النحو التالي: وزارة التربية والتعليم والعلوم والتكنولوجيا. (2023م). مقررا للغة العربية للمرحلة الابتدائية. مؤسسة تنزانيا للتربية .  
جميع الحقوق محفوظة. لا يجوز إعادة إنتاج المقرر أو تخزينه في أي نظام استرجاعي أو نقله أو تفسيره بأي شكل أو بأية طريقة دون إذن مسبق من مؤسسة تنزانيا  
للتربية.

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN: 978-9987-09-835-4

Taasisi ya Elimu Tanzania

Eneo la Mikocheni

132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

S.L.P 35094

14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170

Baruapepe: [director.general@tie.go.tz](mailto:director.general@tie.go.tz)

Tovuti: [www.tie.go.tz](http://www.tie.go.tz)

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Lugha ya Kiarabu Elimu ya Msingi*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

## المحتويات

vii	قائمة الجداول
viii	قائمة الملخصات
ix	الشكر والتقدير
1	1.0 المقدمة
2	2.0 الأهداف العامة للتعليم في تنزانيا
3	3.0 أهداف التعليم الابتدائي من الصف الثالث - السادس
4	4.0 المهارات العامة للتعليم الابتدائي
6	5.0 الكفايات العامة والخاصة
8	6.0 دور المعلمين والتلاميذ والآباء في تعليم وتعلم اللغة العربية
8	6.1 المعلم
10	6.2 التلميذ
11	6.3 الوالد / الوصي
11	7.0 أساليب التدريس المقترحة
12	8.0 الوسائل التعليمية والتعلمية
13	9.0 التقويم في التعليم والتعلم
14	10.0 عدد الحصص
14	11.0 محتوى التعليم والتعلم
69	قائمة المراجع

## Yaliyomo

Orodha ya Majedwali.....	vii
Vifupisho.....	viii
Shukurani.....	x
1.0 Utangulizi.....	1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania.....	2
3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III–VI.....	4
4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la III–VI.....	5
6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji.....	8
6.1 Mwalimu.....	9
6.2 Mwanafunzi.....	10
6.3 Mzazi/Mlezi.....	11
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji.....	12
8.0 Zana/Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji.....	12
9.0 Upimaji katika Ufundishaji na Ujifunzaji.....	13
10.0 Idadi ya vipindi.....	14
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji.....	14
Bibliografia.....	69

## قائمة الجداول

6	الجدول رقم 1: الكفايات العامة والكفايات الخاصة
15	الجدول رقم 2: محتوى الصف الثالث
29	الجدول رقم 3: محتوى الصف الرابع
56	الجدول رقم 4: محتوى الصف الخامس
70	الجدول رقم 5: محتوى الصف السادس

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi	6
Jedwali Na. 2: Maudhui ya Darasa la III	15
Jedwali Na. 3: Maudhui ya Darasa la IV	29
Jedwali Na. 4: Maudhui ya Darasa la V	56
Jedwali Na. 5: Maudhui ya Darasa la VI	70

## قائمة الملخصات

TET	مؤسسة تنزانيا للتربية
TEHAMA	تكنولوجيا المعلومات والاتصالات
LAT	لغة الإشارة في تنزانيا

## Vifupisho

TET	Taasisi ya Elimu Tanzania
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
LAT	Lugha ya Alama Tanzania

## الشكر والتقدير

شارك في إعداد مقرر اللغة العربية للمرحلة الابتدائية من الصف III - VI عدد من الخبراء من المؤسسات الحكومية وغير الحكومية. تقرر وتقدر مؤسسة تنزانيا للتربية (TET) مساهمة جميع المشاركين في إنجاز هذا المقرر. أيضا تود مؤسسة تنزانيا للتربية أن تتقدم بخالص الشكر والتقدير لجميع هؤلاء المتخصصين الذين شاركوا في تطوير هذا المقرر ، بما في ذلك المحاضرين والمدربين ومراقبي الجودة الشاملة للمدارس والمعلمين ومطوري المناهج من TET. كما تقدّم المؤسسة الشكر و التقدير للجنة الفنية الوطنية التي عينها وزير التربية والتعليم والعلوم والتكنولوجيا للإشراف على عملية مراجعة المناهج لمرحلة الأساسية والابتدائية والثانوية وتدريب المعلمين. فقد وفّت اللجنة بالتزاماتها بطريقة احترافية من خلال التأكد من أن هذا المقرر يزود الخريجين بالمهارات والمعرفة التي تمكنهم من العمل لحسابهم الخاص ، والتوظيف ، والقدرة على إدارة حياتهم اليومية، وهو ما يتماشى مع الهدف الأساسي لمراجعة المناهج الدراسية لعام 2023م

أخيرًا ، تقدم TET شكرًا خاصًا لوزارة التربية والتعليم والعلوم والتكنولوجيا لتيسير إعداد وتوزيع هذا المقرر.



Dkt. Aneth A. Komba

المديرة العامة  
مؤسسة تنزانيا للتربية



## Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Lugha ya Kiarabu Elimu ya Msingi darasa la III-VI yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala. Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu kwa Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndio lengo kuu la maboresho ya mitaala ya mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukrani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba  
Mkurugenzi Mkuu  
Taasisi ya Elimu Tanzania

## 1.0 المقدمة

اللغة العربية مادة اختيارية في المرحلة الابتدائية من الصف الثالث إلى السادس. الهدف من تعليم هذه مادة هو تمكين التلميذ من القدرة على الاستماع والقراءة والتحدث والكتابة باللغة العربية، وبناء القدرة على استخدام اللغة بسهولة وفقاً لاحتياجات الاتصال في سياقات مختلفة. تفتح هذه اللغة العديد من الفرص بما في ذلك أن يكون الدارس موظفاً رسمياً أو توظيفاً ذاتياً. كما يمكن هذا الدرس التلميذ من إتقان المهارات الأساسية لمقارنة مفردات اللغة العربية وقواعدها باللغات الأخرى.

تم إعداد هذا المقرر إرشاداً للمعلم في تعليم وتعلم اللغة العربية من الصف الثالث إلى السادس في تنزانيا. يوضح هذا المقرر منهج التعليم الابتدائي لعام 2023م. بالإضافة إلى ذلك، يمكن المقرر المعلم من تخطيط أنشطة التعليم والتعلم من خلال بناء مهارات التلميذ المتمثلة في مهارات التعلم الذاتي والإبداع والتعاون والتواصل وحل التحديات في بيئته.

### 1.0 Utangulizi

Lugha ya Kiarabu ni somo chaguzi katika ngazi ya Elimu ya Msingi kuanzia Darasa la III–VI. Lengo la kufundisha somo hili ni kumwezesha mwanafunzi kuwa na umahiri wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiarabu, na kumjengea uwezo wa kutumia lugha hiyo kwa urahisi kulingana na mahitaji ya mawasiliano katika miktadha mbalimbali. Lugha hii inafungua fursa mbalimbali zikiwemo za kujijajiri na kuajiriwa. Vilevile, somo hili litamwezesha mwanafunzi kumudu stadi za awali za kulinganisha msamiati na sarufi za Lugha ya Kiarabu na lugha nyingine.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiarabu, Darasa la III-VI Tanzania Bara. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023. Aidha, Muhtasari utamwezesha mwalimu kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwanafunzi stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake.

## 2.0 الأهداف العامة للتعليم في تنزانيا

تتمثل الأهداف الرئيسية في تمكين كل تنزاني من:

- (أ) تطوير شخصيته وتحسينها حتى يقدر على احترام نفسه ويثق بنفسه؛
- (ب) احترام ثقافة تنزانيا وتقاليدها وعاداتها والاختلافات الثقافية والتزام وحقوق الإنسان؛ والاتجاهات والتصرفات العامة؛
- (ج) زيادة المعرفة واستخدام العلوم والتكنولوجيا والإبداع والتفكير النقدي والابتكار والتعاون والاتصال والاتجاهات الإيجابية من أجل تنميته والتنمية المستدامة للأمة والعالم بأسره؛
- (د) فهم وحماية القيم الوطنية، بما في ذلك الرأفة والوطنية والأخلاق والوحدة والشفافية والأمانة وتحمل المسؤولية واللغة الوطنية؛
- (هـ) بناء المهارات الحياتية والمتصلة بالعمل من أجل زيادة الكفاءة في الحياة اليومية؛
- (و) تطوير عادة الإعجاب بالعمل وتقييمه من أجل زيادة الإنتاجية والكفاءة في الإنتاج وتقديم الخدمات؛
- (ز) تحديد القضايا الاجتماعية الشاملة والعناية بها، بما في ذلك صحة ورفاهية الأشخاص الآخرين (المجتمع)، والمساواة الجنسية، وكذلك إدارة البيئة والحفاظ عليها بشكل مستديم؛ و
- (ح) تطوير التعاون الوطني والدولي والسلام والعدالة وفقا للدستور والاتفاقيات الدولية.

### 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

- (a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
- (b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Kitanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

- (c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
- (d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;
- (e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
- (f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
- (g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
- (h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

### 3.0 أهداف التعليم الابتدائي من الصف الثالث - السادس

تضمن أهداف التعليم الابتدائي من الصف الثالث إلى السادس في تمكين الطالب من:

- (أ) تنمية مهارات القراءة والكتابة والحساب والتواصل بلغة صحيحة وطلاقة، ولغة الإشارة التنزانية ولغة اللمس
- (ب) معرفة واستخدام وتقدير اللغة السواحيلية والإنجليزية بالإضافة إلى لغة أجنبية واحدة أخرى على الأقل (اللغة العربية واللغة الفرنسية واللغة الصينية)
- (ج) تقدير الثقافة التنزانية والوحدة الوطنية والاعتراف بالثقافات الأخرى والحفاظ عليها؛
- (د) تنمية المعرفة والقدرة على الاستفسار والتفكير الإيجابي، والإبداع إضافة إلى تقديم حلول مناسبة للمشكلات؛
- (هـ) تعزيز القيم والنزاهة واحترام الاختلاف في الأديان؛
- (و) تحديد وتطوير المواهب ومهارات العمل والرياضة والفنون؛
- (ز) تنمية عادة حب العمل وتقديره؛
- (ح) معرفة العلوم والتكنولوجيا وتوظيفهما في التعلم والحياة اليومية؛

(ط) تنمية المعارف والمهارات والاتجاهات في الاهتمام بالبيئة والمحافظة عليها واحترام المساواة بين الجنسين وغير ذلك من القضايا الشاملة؛

(ي) تطوير القدرة على التداخل والتمسك الاجتماعي في بيئة شاملة.

### 3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III–VI

Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa III–VI ni kumwezesha mwanafunzi:

- (a) Kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;
- (b) Kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha nyingine moja ya kigeni;
- (c) Kuthamini na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;
- (d) Kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;
- (e) Kukuza maadili, uadilifu na kuheshimu tofauti za imani;
- (f) Kubaini na kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;
- (g) Kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi;
- (h) Kutambua na kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;
- (i) Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na
- (j) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

### 4.0 الكفاءات العامة للتعليم الابتدائي

الكفاءات العامة التي سيبنيها التلميذ من الصف الثالث إلى السادس هي:

- (أ) استخدام مهارات القراءة والكتابة والحساب والتواصل بطلاقة، ولغة الإشارة في تنزانيا (LAT) ولغة اللمس.
- (ب) استخدام اللغة السواحيلية والإنجليزية ولغة أجنبية أخرى وتقديرها؛
- (ج) احترام الثقافة التنزانية، والوحدة الوطنية والاعتراف بالثقافات الأخرى؛

- (د) التحلي بالفضول والتفكير الواقعي، والإبداع، وتقديم الحلول المناسبة للمشكلات؛
- (هـ) إظهار العدالة والنزاهة واحترام الاختلاف العقيدي.
- (و) توظيف المواهب ومهارات العمل والرياضة والفنون في ميادين مختلفة؛
- (ز) تقدير وحب العمل؛
- (ح) توظيف العلوم والتكنولوجيا في عملية التعلم وفي مواقف الحياة اليومية؛
- (ط) الاهتمام بالمحافظة على البيئة واحترام المساواة بين الجنسين وغير ذلك من القضايا الشاملة؛
- (ي) تنمية فكرة التداخل الاجتماعي الإيجابي والمشاركة في قضايا الاجتماعية الشاملة.

#### 4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la III–VI

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasa la III–VI ni:

- (a) Kutumia stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;
- (b) Kutumia na kuithamini lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha nyingine moja ya kigeni kulingana na hali halisi ya shule yake;
- (c) Kuonesha, kuthamini na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;
- (d) Kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;
- (e) Kuonesha uadilifu na kuheshimu tofauti za imani;
- (f) Kutumia vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa katika miktadha mbalimbali;
- (g) Kuthamini na kupenda kufanya kazi;
- (h) Kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;
- (i) Kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na
- (j) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

**5.0 الكفايات العامة والكفايات الخاصة**  
 الكفايات العامة و الكفايات الخاصة التي سيتم تطويرها موضحة في الجدول 1  
 الجدول رقم I: الكفايات العامة والكفايات الخاصة.

**Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa kwa Darasa la III - VI umebainishwa katika Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na.1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi**

الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
1.1 القدرة على إتقان فهم الأصوات ونطق الحروف العربية وكتابتها 1.1 Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya herufi za Kiarabu na uandishi wake	1.0 القدرة على إتقان المهارات الأساسية للغة العربية 1.0 Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kiarabu
1.2 ربط الكلمات بالأشياء في البيئة 1.2 Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira	
1.3 القدرة على إتقان القواعد والمفردات السهلة 1.3 Kumudu sarufi na msamiati sahili	

الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
2.1 Kusikiliza na kuelewa taarifa	2.0 إظهار فهم المعلومات في المحادثة والكتابة
2.2 Kusoma na kuelewa matini sahili	2.0 Kuonesha uelewa wa taarifa katika mazungumzo na maandishi
2.3 Kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika	
2.4 Kusoma kwa usahihi aina mbalimbali za matini sahili	
3.1 Kuonesha uelewa wa sifa za msingi za lugha ya mazungumzo na maandishi	3.0 التوصل الفعال في السياقات المختلفة
	3.0 Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali



## 6.0 دور المعلمين والتلاميذ والآباء في تعليم وتعلم اللغة العربية

يعتمد التعليم والتعلم على التعاون الفعال بين المعلم والتلاميذ وولي الأمر / الوصي. واجباتهم على النحو التالي:

### 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

#### 6.1 المعلم

- (أ) تمكين التلميذ من التعلم واكتساب الكفاءة المقصودة في اللغة العربية؛
- (ب) استخدام اساليب التعليم والتعلم على أساس العمر وقدرته واحتياجاته المختلفة التي ستمكن الطالب من:
  - (i) بناء الكفاءات المطلوبة في القرن الحادي والعشرين (21)؛
  - (ii) المشاركة الفعالة في عملية التعلم
- (ج) استخدام اساليب المشاركة التي تجعل الطالب مركز التعلم، بما في ذلك التي ستمكنه من التفكير وطلب المعرفة من مصادر مختلفة. تشمل طرق المقترحة لتعلم وتعليم والبحث والتجارب العلمية والمناقشة وعمل المشروع التي تهدف إلى حل المشكلات الحقيقية في بيئة الطالب. بالإضافة إلى ذلك، يتم تشجيع المعلم على استخدام مثل هذه أساليب أخرى شبيهة بهذه وفقاً للسياق من أجل تحقيق بناء الكفاءة المقصودة.
- (د) تهيئة فصل آمن ذي جو ملائم للتعليم والتعلم؛
- (هـ) تطوير أدوات التعليم والتعلم وتقييمها
- (و) إجراء اختبار دوري باستخدام أدوات وأساليب الاختبار والتقييم التي تقيس النظرية والممارسة بما في ذلك العصف الذهني، وقوائم المراجعة، والاختبارات، والاستبيانات، والتمارين (العمل الفردي، والعمل الجماعي)، والمشروع. الأدوات والأساليب الأخرى هي الاختبارات العملية والعروض التقديمية وامتحانات منتصف الفصل والامتحانات النهائية؛

- (ز) التأكد من أن عملية التعلم والتعليم تتم بشكل عادل ومتساوٍ لكل تلميذ دون النظر إلى اختلافاتهم
- (ح) تحديد احتياجات الطالب وتقديم الحل المناسب؛
- (ط) حماية الطالب إذا كان في المدرسة
- (ي) متابعة تحسين التلميذ اليومي
- (ك) إشراك الآباء/الأوصياء والمجتمع في مختلف مراحل تعلم الطلاب
- (ل) دمج القضايا الشاملة وتكنولوجيا المعلومات والاتصالات في عملية التعليم والتعلم.

## 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

- (a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika lugha ya Kiarabu;
- (b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wa mwanafunzi zitakazomwezesha:
- (i) Kujenga umahiri uliokusudiwa katika Karne ya 21;
- (ii) Kushiriki kikamilifu katika tendo zima la ujifunzaji.
- (c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zitakazomwezesha kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Njia za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na kazi za vitendo, utafiti, majaribio ya kisayansi, majadiliano na kazi mradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha mwalimu anahimizwa kutumia njia nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa;
- (d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;
- (e) Kutengeneza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

- (f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi, kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;
- (g) Kuhakikisha kuwa tendo la ujifunzaji na ufundishaji linafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;
- (h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;
- (i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;
- (j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;
- (k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na
- (l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

## 6.2 التلميذ

يتوقع من التلميذ:

- (أ) أن يكون رئيساً تنفيذياً في عملية التعلم بأكملها
- (ب) لاكتساب الكفاءة المقصودة من خلال المشاركة في أنشطة التعلم المختلفة داخل الفصل وخارجه؛ و
- (ج) المشاركة في العثور على المعرفة من مصادر مختلفة بما في ذلك الكتب المدرسية والملاحق والمنشورات الأخرى من المكتبة الإلكترونية.

## 6.2 Mwanafunzi

### Mwanafunzi anatarajiwa:

- (a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;
- (b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa; na
- (c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktaba mtandao

### 6.3 الوالد / الوصي

من المتوقع من الوالد/الوصي:

- (أ) الإشراف ومتابعة تقدم الولد في التعلم
- (ب) الإشراف على الولد لأداء واجباته المهنية حيثما أمكن
- (ج) التأكد من أن بيئة المنزل صديقة وآمنة تسهل التعلم
- (د) تتبع و مراقبة سلوك الولد
- (هـ) تزويد الولد بجميع المواد المطلوبة في عملية التعلم
- (و) التأكد من أن الولد يحصل على الاحتياجات اللازمة
- (ز) توعية الولد بأهمية التعليم وقيمه وتشجيعه على التعليم الجاد

### 6.3 Mzazi/Mlezi

**Mzazi/Mlezi anatarajiwa:**

- (a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;
- (b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;
- (c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayoweza ujifunzaji
- (d) Kufuatilia mwenendo wa kitabia wa mtoto;
- (e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika shughuli ya ujifunzaji;
- (f) Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na
- (g) Kumfundisha mtoto kuhusu umuhimu na thamani ya elimu pamoja na kumhimiza kujifunza kwa bidii.

### 7.0 أساليب التدريس المقترحة

تعتبر أساليب التعليم والتعلم أساسية في بناء الكفاءة لدى الطالب. يقترح هذا المقرر أساليب التعلم والتعليم لكل نشاط؛ منها الزيارات الأكاديمية، والأعمال، والسرود، والمناقشات، والتفكير، والكتابة، والمشاركة الزوجية، وعمل المشروع. ومع ذلك، يُنصح المعلم باستخدام أساليب أخرى من هذا القبيل اعتمادًا على سياق التعليم والتعلم

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu unapendekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni ziara za kimasomo, kazi za vitendo, masimulizi, majadiliano, fikiri-andika-jozisha-shirikisha na kazimradi. Hata hivyo, mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 8.0 الوسائل التعليمية والتعلمية

عملية التعليم والتعلم تتطلب مجموعة متنوعة من الأدوات لبناء الكفاءة المستهدفة. لذلك، يجب على المعلم والتلميذ التعاون في تحديد وتقييم الأدوات البديلة المتاحة في البيئة المدرسية وفي المنزل عند الحاجة. يجب على المعلم والتلميذ البحث عن المعلومات من مصادر متعددة لتحقيق كفاءة في عمليات التعليم والتعلم. ستقدم قائمة بالكتب المعتمدة لاستخدامها كمراجع من قبل مؤسسة تنزانيا للتربية.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana/vifaa mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana/vifaa mbadala vinavyopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi vinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutumika kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

## 9.0 التقويم في التعليم والتعلم

التقويم هو قضية مهمة في عملية التعلم والتعليم لتسهيل بناء الكفاءة المقصودة. سيُشمل تقييم اللغة العربية تقييمًا مستمرًا وتقييمًا نهائيًا. سيأخذ التقييم المستمر في الاعتبار المعايير المحددة في كل نشاط تعليمي وسيتمكن المعلم من تحديد قدرة التلميذ وحاجته في التعلم. بالإضافة إلى ذلك، سوف تهدف إلى قياس التغييرات في المعرفة والمهارات والتجاه إلى التصرف والتقدير والسرور واستخدام المهارات التي يتعلمها في البيئة المحيطة به. بالإضافة إلى ذلك، سيستخدم المعلم معلومات الاختبار لتحسين التدريس وتمكين التلميذ من تحقيق هدف التعلم. أدوات التقييم التي يمكن استخدامها في أنشطة التعليمية هي العصف الذهني، وقوائم المراجعة، والتمارين الصفية، والاختبارات، والاختبارات العملية، والاستبيانات، والأسئلة وجهًا لوجه، والتمارين، والعمليات (العمل الفردي والجماعي)، والمشاريع وحقبة العمل وغيرها.

سيشمل التقييم النهائي امتحانات أسبوعية وفصلية ونهاية العام الدراسي والتي سيتم استخدامها لقياس تقدم تعلم الطلاب. سيتم استخدام المعلومات من هذا التقييم لمعرفة مدى تقدم الطالب، وتقديم التغذية الراجعة لتسهيل التدريس والتعلم. بالإضافة إلى ذلك، سيكون هناك امتحان وطني للنموذج السادس والذي سيساهم بـ ٧,٥ نقطة في امتحان الصف الرابع الثانوي.

### 9.0 Upimaji katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Upimaji ni suala muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji ili kuwezesha ujenzi wa umahiri unaokusudiwa. Upimaji wa lugha ya Kiarabu utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Vilevile, utalenga kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Aidha, mwalimu atatumia taarifa za upimaji kuboresha ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufikia lengo la ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodha hakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana

kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo. Upimaji tamati utahusisha mitihani ya wiki, muhula na mtihani wa mwisho wa mwaka ambayo itatumika kupima maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Taarifa za upimaji huu pamoja na kutumika kutathimini maendeleo ya mwanafunzi, zitatumika kutoa mrejesho wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, kutakuwa na upimaji wa kitaifa wa Darasa la Sita ambao utachangia alama 7.5 katika mtihani wa Kidato cha Nne.

### 10.0 عدد الحصص

يقدم مقرر اللغة العربية للتعليم الابتدائي تقديرات للوقت الذي سيتم قضاؤه في التعليم و التعلم. نظرًا لكثرة الكفاءات الخاصة وأنشطة التعلم، تم تخصيص حصتين في الأسبوع، لكل منهما أربعون دقيقة.

### 10.0 Idadi ya vipindi

Muhtasari wa Kiarabu Elimu ya Msingi Darasa la III – VI unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni viwili (2) kwa wiki.

### 11.0 محتوى التعليم والتعلم

يحتوي مقرر اللغة العربية للصف الثالث الابتدائي إلى السادس على محتوى منظم في سبعة عناصر متمثلة في الكفاية العامة، والخاصة، وأنشطة الطالب، والطرق المقترحة، ومعايير التقييم، والوسائل التعليمية والتعلمية، بالإضافة إلى عدد الحصص.

### 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Kiarabu Elimu ya Msingi Darasa la III -VI umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele saba ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu pendekezwa, vigezo vya upimaji, zana/vifaa pamoja na idadi ya vipindi kama inavyowasilishwa katika Jedwali Na. 2 – 5.

الثالث الابتدائي: Darasa la III

Jedwali Na. 2: Maudhui ya Darasa la III

الجدول رقم 2: محتوى الصف III

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعلمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
14	المسجلات الصوتية المتخصصة في مهارة الاستماع و الكلام  Vinasa sauti vyenye maudhui au mada za stadi za kusikiliza na kuzungumza	تم الاستماع والنطق بالأصوات العربية بطريقة صحيحة  Sauti za Kiarabu zimesikilizwa na kutamkwa kwa usahihi	دراسة حالة: وجه التلاميذ للاستماع إلى أصوات اللغة العربية  <b>Kisamafunzo:</b> Waongoze wanafunzi kusikiliza sauti za lugha ya Kiarabu  <b>عمل جماعي:</b> أعين التلاميذ على التعرف على أصوات اللغة العربية  <b>Kazi ya vikundi:</b> Waongoze wanafunzi kuelewa sauti za lugha ya Kiarabu.	(أ) استماع الأصوات العربية ونطقها (a) Kusikiliza na kutamka sauti za Kiarabu	1.1 القدرة على إتقان فهم الأصوات ونطق الحروف العربية وكتابتها  1.1 Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya herufi za Kiarabu na uandishi wake	1.0 القدرة على إتقان المهارات الأساسية للغة العربية  1.0 Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kiarabu



عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
			<p>المناقشة الجماعية: أرشد التلاميذ لمناقشة أصوات مختلفة والتمييز بينها نطقاً</p> <p><b>Majadiliano ya vikundi:</b> Waongoze wanafunzi kujadili sauti mbalimbali za lugha ya kiarabu na kuzitofautisha kimatamshi.</p>			
	النصوص المتنوعة المتخصصة في القراءة والكتابة  Matini anuai zilizojikita katika maudhui za kusoma na kuandika	قُرئت الحروف العربية وكتبت بطريقة صحيحة  Konsonanti za Kiarabu zimesomwa na zimeandikwa kwa usahihi	<p>التكرار أرشد التلاميذ إلى قراءة الحروف العربية</p> <p><b>Kukariri</b> Waongoze wanafunzi kusoma konsonanti za Kiarabu.</p> <p>نسخ أرشد التلاميذ على كتابة الحروف العربية</p> <p><b>Kunukuu</b> Waongoze wanafunzi kuandika konsonanti za Kiarabu.</p>	(ب) قراءة الحروف العربية وكتابتها  (b) Kusoma na kuandika konsonanti za Kiarabu		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
	<p>المسجلات الصوتية المتخصصة في مهارة الاستماع و الكلام</p> <p>Vinasa sauti vyenye maudhui au mada za stadi za kusikiliza na kuzungumza</p>	<p>تم الاستماع والنطق بالحركات العربية بطريقة صحيحة</p> <p>Irabu za Kiarabu zimesikilizwa na kutamka kwa usahihi</p>	<p><b>العرض:</b> أرشد التلاميذ للتعرف على حركات اللغة العربية</p> <p><b>Oneshombinu:</b> Waongoze wanafunzi kuzitambua irabu za lugha ya kiarabu.</p> <p><b>المناقشة الجماعية:</b> أرشد التلاميذ لمناقشة الحركات العربية</p> <p><b>Majadiliano ya vikundi:</b> Waongoze wanafunzi kujadili irabu za lugha ya kiarabu.</p> <p><b>التكرار:</b> أرشد التلاميذ لنطق الحركات العربية</p> <p><b>Kukariri:</b> Waongoze wanafunzi kutamka irabu za Kiarabu.</p>	<p>(ج) استماع الحركات العربية ونطقها</p> <p>(c) Kusikiliza na kutamka irabu za Kiarabu</p>		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعلمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
	النصوص المتنوعة المتخصصة في مهارة القراءة والكتابة  Matini mbalimbali zenye maudhui za kusoma na kuandika	قُرئت الحركات العربية وَكُنبت بطريقة صحيحة  Irabu za Kiarabu zimesomwa na zimeandikwa kwa usahihi	زيارة الكلري: أرشد التلاميذ للتعرف على أشكال الحركات المختلفة  <b>Matembezi ya galari:</b> Waongoze wanafunzi kutambua maumbo mbalimbali ya irabu za Kiarabu.  المناقشة الجماعية: أرشد التلاميذ لمناقشة أشكال الحركات المختلفة  <b>Majadiliano ya vikundi:</b> Waongoze wanafunzi kujadili maumbo mbalimbali ya irabu za Kiarabu.  العرض: أرشد التلاميذ لكتابة الحركات العربية  <b>Oneshombinu:</b> Waongoze wanafunzi kuandika irabu za Kiarabu	(د) قراءة الحركات العربية وكتابتها  (d) Kusoma na Kuandika irabu za Kiarabu		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
		قُرئت المقاطع العربية وكتبت بطريقة صحيحة  Silabi za Kiarabu zimesomwa na zimeandikwa kwa usahihi	<b>بطاقات الكلمات</b> أرشد الطلاب لقراءة المقاطع في البطاقات المعدة  <b>Kadi za silabi/maneno</b> Waongoze wanafunzi kusoma silabi katika kadi zilizoandaliwa	(هـ) قراءة المقاطع العربية المختلفة وكتابتها  (e) Kusoma na kuandika silabi mbalimbali za Kiarabu		
12	المنشورات المتنوعة ذات أسماء وكلمات الأشياء المختلفة  Machapisho mbalimbali yenye majina na maneno ya vitu anuai	تحقق التعرف على أسماء الأشياء الموجودة في الصف Majina ya vitu vya darasani yametambuliwa kwa usahihi تحقق التعرف على أسماء الأشياء الموجودة في بيئة المدرسة Majina ya vitu vinavyopatikana katika mazingira ya shule yametambuliwa kwa usahihi	<b>العصف الذهني</b> أرشد التلاميذ للتعرف على أسماء الأشياء الموجودة في الفصل  <b>Bunguabongo</b> Waongoze wanafunzi kutambua majina ya vitu vya darasani  <b>زيارة الكلري</b> أرشد التلاميذ لبيان أسماء الأشياء الموجودة في بيئة المدرسة  <b>Matembezi ya galari</b> Waongoze wanafunzi kutambua majina ya vitu vinavyopatikana katika mazingira ya shule	(أ) الربط بين الكلمات والأشياء الموجودة في الصف وفي البيئة المدرسية  (a) Kuhusianisha maneno na vitu mbalimbali vinavyopatikana darasani na mazingira ya shule	1.2 ربط الكلمات بالأشياء في البيئة  1.2 Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira	

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعلمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
	المنشورات المتنوعة ذات كلمات وأفعال  Machapisho mbalimbali yenye maneno na vitendo	حصل التعرف على الأفعال التي تحدث في الفصل بشكل صحيح  Vitendo mbalimbali vinavyofanyika darasani vimetambuliwa kwa usahihi  حصل التعرف على الأفعال التي تحدث في بيئة المدرسة بشكل صحيح  Vitendo mbalimbali vinavyofanyika katika mazingira ya shule vimetambuliwa kwa usahihi	زيارة الكلري أرشد التلاميذ لبيان الأفعال التي تحدث في الفصل  <b>Matembezi ya galari</b> Waongoze wanafunzi kubaini vitendo vinavyofanyika katika mazingira ya darasani  لعِب الأدوار أرشد التلاميذ لبيان الأفعال التي تحدث في بيئة المدرسة  <b>Igizodhima</b> Waongoze wanafunzi kubaini vitendo mbalimbali vinavyofanyika katika mzingira ya shuleni.	(ب) الربط بين الكلمات والأفعال التي تحدث في الصف وفي البيئة المدرسية  (b) Kuhusianisha maneno na vitendo mbalimbali vinavyofanyika darasani na katika mazingira ya shule		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعلمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
	النصوص المتنوعة المتخصصة في القراءة  Matini anuai zenye maudhui ya kusoma	فُرئت أسماء الأشياء والأفعال التي تقع في الصف وفي البيئة المدرسية بطريقة صحيحة  Maneno yanayohusianisha vitu na vitendo vinavyofanyika darasani yamesomwa kwa usahihi	<b>المناقشة الجماعية:</b> أرشد التلاميذ لقراءة أسماء الأشياء والأفعال التي تقع في الفصل  <b>Majadiliano ya vikundi</b> Waongoze wanafunzi kusoma maneno yanayohusianisha vitu na vitendo vinavyofanyika katika mazingira ya darasani.  <b>لعِب الأدوار</b> أرشد التلاميذ للمشاركة في قراءة أسماء الأشياء والأفعال التي تقع في البيئة المدرسية  <b>Igizodhima</b> waongoze wanafunzi kushiriki katika igizo la kusoma maneno yanayohusianisha vitu na vitendo vinavyofanyika katika mazingira ya shuleni.	(ج) قراءة الكلمات المتعلقة بالأشياء والأفعال التي تقع في الصف وفي البيئة المدرسية  (c) Kusoma maneno yanayohusianisha vitu na vitendo vinavyofanyika katika mazingira ya darasani na shuleni		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعلمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
	النصوص المتنوعة المتخصصة في الكتابة  Matini anuai zenye maudhui ya kuandika	كُتِبَتْ أسماء الأشياء والأفعال التي تقع في الصف وفي البيئة المدرسية بطريقة صحيحة  Maneno yanayohusianisha vitu na vitendo vinavyofanyika darasani yameandikwa kwa usahihi	<b>المناقشة الجماعية:</b> أرشد التلاميذ من كتابة أسماء الأشياء والأفعال التي تقع في الفصل  <b>Majadiliano ya vikundi:</b> Waongoze wanafunzi kuandika maneno yanayohusianisha vitu na vitendo vinavyofanyika katika mazingira ya darasani.  <b>العرض</b> أرشد التلاميذ لكتابة أسماء الأشياء والأفعال التي تقع في البيئة المدرسية  <b>Oneshombinu</b> Waongoze wanafunzi kuandika maneno yanayohusianisha vitu na vitendo vinavyofanyika katika mazingira ya shuleni	(د) كتابة الكلمات المتعلقة بالأشياء والأفعال التي تقع في الصف وفي البيئة المدرسية  (d) Kuandika  maneno yanayo husianisha vitu na vitendo vinavyofanyika katika mazingira ya darasani na shuleni		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
12	المسجلات الصوتية المتخصصة في مهارة الكلام  Vinasa sauti vyenye mada au maudhui za kuzungumza	عرّف التلاميذ أنفسهم بفصاحة ووضوح  Wanafunzi wamejitambulisha kwa usahihi	<b>الحوار</b> أرشد التلاميذ إلى التعريف الشخصي  <b>Dayalojia</b> Waongoze wanafunzi kujitambulisha	(أ) التعريف الشخصي باستخدام جمل سهلة  (a) Kujitambulisha kwa kutumia sentensi sahili	1.3 القدرة على إتقان القواعد والمفردات السهلة 1.3 Kumudu sarufi na msamiati sahili	
	منشورات متنوعة مستعملة في قراءة وكتابة الكلمات  Machapisho mbalimbali yenye maudhi za kusoma na kuandika maneno	قُرئت الكلمات المستخدمة في التعريف الشخصي وكُنيت بطريقة صحيحة  Maneno yanayotumika katika kujitambulisha yamesomwa na kuandikwa kwa usahihi	<b>العرض</b> أرشد التلاميذ لقراءة وكتابة الكلمات المستخدمة في التعارف  <b>Oneshombinu</b> Waongoze wanafunzi kusoma na kuandika maneno yanayotumika katika kujitambulisha	(ب) قراءة الكلمات المستخدمة في التعريف الشخصي وكتابتها  (b) Kusoma na kuandika maneno yanayotumika katika kujitambulisha		



عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعلمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
	المنشورات والنصوص المختلفة عن الأوقات والأزمنة  Machapisho na matini anuai yenye maudhui za kusoma wakati	تم التعبير الصحيح عن الأوقات والأزمنة  Aina mbalimbali za nyakati zimebainishwa kwa usahihi	<b>لعِب الأدوار</b> أرشد التلاميذ لبيان الأوقات والأزمنة المختلفة  <b>Igizombinu</b> Waongoze wanafunzi kubaini aina mbalimbali za nyakati.	(ج) التعبير عن الأوقات والأزمنة المختلفة  (c) Kubaini nyakati mbalimbali		
12	المسجلات الصوتية المتخصصة في مهارة الاستماع  Vinasa sauti vyenye mada au maudhui za kusikiliza	حصلت استجابة التحايا والدعوات والوداع والشكر شفويًا بطريقة سوية  Mazungumzo kuhusu maamkizi, mialiko, maagano na shukrani yamefanyika kwa usahihi	<b>الحوار</b> أرشد التلاميذ للتعرف على الكلمات المستخدمة في التحايا والدعوات والوداع والشكر  <b>Dayalojia</b> Waongoze wanafunzi kutambua maneno mbalimbali yanayotumika katika salamu, mwaliko, kuagana na kushukur	(أ) استجابة التحايا والدعوات والوداع والشكر شفويًا  (a) Kusikiliza na kujibu salamu, mwaliko, kuagana na shukurani	2.1 الاستماع والفهم المعلومات  2.1 Kusikiliza na kuelewa taarifa	2.0 إظهار فهم المعلومات في المحادثة والكتابة  2.0 Kuonesha uelewa wa taarifa katika mazungumzo na maandishi

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعلمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
			<p><b>عمل جماعي:</b> أرشد التلاميذ لبيان أساليب مختلفة في تبادل التحايا والدعوات والوداع والشكر</p> <p><b>Kazi za vikundi:</b> Waongoze wanafunzi kubaini aina mbalimbali za kuitikia salamu, mwaliko, kuagana na shukrani.</p> <p><b>الحوار:</b> أرشد التلاميذ لردّ التحية وإجابة الدعوة وتبادل تعبيرات الوداع والشكر</p> <p><b>Dayalojia:</b> Waongoze wanafunzi kujibu kwa usahihi salamu, mwaliko, kuagana na shukrani</p>			

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
		<p>حصلت استجابة والرد على التعليمات السهلة المقدمة في المدرسة شفويًا بطريقة صحيحة</p> <p>Maelekezo sahili yanayotolewa shuleni yamefanyika kwa usahihi</p>	<p><b>الحوار:</b> أرشد التلاميذ للتعرف على التعليمات السهلة المقدمة في المدرسة</p> <p><b>Dayalojia:</b> Waongoze wanafunzi kutambua maelekezo sahili yanayotolewa shuleni</p> <p><b>عمل جماعي:</b> أرشد التلاميذ لاستخدام الأنواع المختلفة من التعليمات السهلة المقدمة في المدرسة</p> <p><b>Kazi za vikundi:</b> Waongoze wanafunzi kutumia aina mbalimbali za maelekezo sahili yatolewayo shuleni</p>	<p>(ب) الاستماع والرد على التعليمات السهلة المقدمة في المدرسة</p> <p>(b) Kusikiliza na kujibu maelekezo sahili yanayotolewa shuleni</p>		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعلمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
6	المسجلات الصوتية المتخصصة في مهارة الاستماع  Vinasa sauti vyenye mada au maudhui za kusikiliza	تمت إجابة الطلبات واتباع التوجيهات السهلة الموجهة في البيئة المدرسية بشكل صحيح  Maagizo na maelekezo sahili yanayotolewa katika mazingira ya shule yamefuatwa kwa usahihi	<b>مسرحية موجزة:</b> أرشد التلاميذ لاستماع واتباع الأوامر والتوجيهات السهلة المتعلقة بالبيئة المدرسية  <b>Igizo fupi:</b> Waongoze wanafunzi kubaini maagizo na maelekezo yanayotolewa shuleni.	(أ) استماع واتباع إلى الطلبات والتوجيهات السهلة الموجهة في البيئة المدرسية واتباعها  (a) Kusikiliza na kufuata maagizo au maelekezo sahili yanayotolewa katika mazingira ya shule	2.2 إظهار الاستجابة الصحيحة في سياق تواصل مألوف  2.2 Kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika	
		تم إبداء الشعور الصحيحة من استماع إلى خبر سهل قصير بشكل صحيح  Hisia sahihi zilizotokana na usikilizaji wa taarifa fupi sahili zimeonyeshwa kwa usahihi	<b>لعبة الأدوار</b> أرشد التلاميذ لاستماع إلى خبر قصير وإبداء الشعور الصحيحة تجاهه  <b>Igizodhima:</b> Waongoze wanafunzi kuonesha hisia sahihi kutokana na taarifa fupi waliyoisikiliza	(ب) الاستماع إلى خبر سهل وقصير وإبداء الشعور الصحيحة  (b) Kusikiliza na kuonesha hisia sahihi kutokana na taarifa fupi sahili		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
14	النصوص المتنوعة المتخصصة في الكلام والكتابة  Matini mbalimbali zenye maudhui ya uwasilishaji kwa njia ya mazungumzo na maandishi	تحقق استخدام التنغيم الصحيح أثناء التواصل  Kiimbo sahihi kimetumika wakati wa kuwasiliana	<b>الحوار</b> أرشد التلاميذ لاستخدام أنواع مختلفة للتنغيم  <b>Dayalojia</b> Waongoze wanafunzi kutumia na kutofautisha aina mbalimbali za viimbo	(أ) استخدام التنغيم الصحيح أثناء التواصل  (a) Kutumia kiimbo sahihi wakati wa kuwasiliana	3.1 فهم الملامح الأساسية للغة المحادثة والنصوص المكتوبة  3.1 Kuonesha uelewa wa sifa za msingi za lugha ya mazungumzo na maandishi	3.0 التواصل الفعال في السياقات المختلفة  3.0 Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali
		استخدمت علامة الاستفهام والنقطة بطريقة صحيحة  Alama za kuuliza na kituo zimetumika kwa usahihi	<b>المناقشة الجماعية:</b> أرشد التلاميذ للتعرف على علامة الاستفهام والنقطة واستعمالهما  <b>Majadiliano ya vikundi:</b> Waongoze wanafunzi kutambua na kutumia alama ya kuuliza na ya kituo	(ب) الاستخدام الصحيح لعلامات الترقيم (علامة الاستفهام والنقطة)  (b) Kutumia alama za uakifishaji kwa usahihi (alama za kuuliza swali na kituo)		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعلمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	الكفايات الخاصة Umahiri mahususi	الكفايات العامة Umahiri mkuu
		استُخدمت علامة التعجب والفاصلة بطريقة صحيحة  Alama za mshangao na mkato zimetumika kwa usahihi	المناقشة الجماعية: أرشد التلاميذ للتعرف على علامة التعجب والفاصلة والاستخدامهما  <b>Majadiliano ya vikundi:</b> Waongoze wanafunzi kutambua na kutumia alama ya mshangao na ya mkato	(ج) الاستخدام الصحيح لعامة الترقيم (علامة التعجب والفاصلة)  (c) Kutumia alama za uakifishaji kwa usahihi (alama za mshangao na mkato)		

الرابع الابتدائي: Darasa la IV

الجدول رقم 3 : محتوى الصف IV

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Darasa la IV

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	المهارات الخاصة Umahiri mahususi	المهارات العامة Umahiri mkuu
10	المسجلات الصوتية المتخصصة في مهارة الاستماع  Vinasau sauti vyenye mada au maudhui ya kusikiliza	تم نطق الكلمات المتحركة بحركات قصيرة بطريقة صحيحة  Maneno yenye irabu fupi yametamkwa kwa usahihi	لعب الأدوار: أرشد التلاميذ لنطق الكلمات المتحركة بحركات قصيرة  <b>Igizodhima:</b> Waongoze wanafunzi kutamka maneno yenye irabu fupi	(أ) الاستماع إلى الكلمات المتحركة بحركات قصيرة ونطقها  (a) Kusikiliza na kutamka maneno yenye irabu fupi	1.1 اكتساب المهارات الأساسية للأصوات ونطق الحروف العربية وكتابتها  1.1 Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya herufi za kiarabu na uandishi wake	1.0 القدرة على إتقان المهارات الأساسية للغة العربية  1.0 Kumudu stadi za msingi za lughu ya Kiarabu

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	المهارات الخاصة Umahiri mahususi	المهارات العامة Umahiri mkuu
		تم نطق الكلمات المتحركة بحركات طويلة بشكل صحيح Maneno yenye irabu ndefu yametamkwa kwa usahihi	<b>لعِب الأدوار:</b> أرشد التلاميذ لنطق الكلمات المتحركة بحركات طويلة <b>Igizodhima:</b> Waongoze wanafunzi kutamka maneno yenye irabu ndefu	(ب) استماع إلى الكلمات المتحركة بحركات طويلة ونطقها (b) Kusikiliza na kutamka maneno yenye irabu ndefu		
		قُرئت الكلمات المتحركة بحركات قصيرة بشكل صحيح Maneno yenye irabu fupi yamesomwa kwa usahihi كُتبت الكلمات المتحركة بحركات قصيرة بشكل صحيح Maneno yenye irabu fupi yameandikwa kwa usahihi	<b>قراءة النص:</b> أرشد التلاميذ لقراءة الكلمات المتحركة بحركات قصيرة <b>Usomaji matini:</b> Waongoze wanafunzi kusoma maneno yenye irabu fupi	(ج) قراءة الكلمات المتحركة بحركات قصيرة وكتابتها (c) Kusoma na kuandika maneno yenye irabu fupi	(ج) قراءة الكلمات المتحركة بحركات قصيرة وكتابتها (c) Kusoma na kuandika maneno yenye irabu fupi	



عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	المهارات الخاصة Umahiri mahususi	المهارات العامة Umahiri mkuu
			<p><b>العرض:</b> أرشد التلاميذ لكتابة الكلمات المتحركة بحركات قصيرة</p> <p><b>Oneshombinu:</b> Waongoze wanafunzi kuandika maneno yenye irabu fupi</p>			
		<p>قُرئت الكلمات المتحركة بحركات طويلة بشكل صحيح</p> <p>Maneno yenye irabu ndefu yamesomwa kwa usahihi</p> <p>كُتبت الكلمات المتحركة بحركات طويلة بشكل صحيح</p> <p>Maneno yenye irabu ndefu yameandikwa kwa usahihi</p>	<p><b>قراءة النص:</b> أرشد التلاميذ لقراءة الكلمات المتحركة بحركات طويلة</p> <p><b>Usomaji matini:</b> Waongoze wanafunzi kusoma maneno yenye irabu ndefu</p> <p><b>ماذا في الحقيقية:</b> أرشد التلاميذ لكتابة الكلمات المتحركة بحركات طويلة</p> <p><b>Mchezo wa kapuni kuna nini:</b> Waongoze wanafunzi kuandika maneno yenye irabu ndefu</p>	(د) قراءة الكلمات المتحركة بحركات طويلة وكتابتها	(d) Kusoma na kuandika maneno yenye irabu ndefu	

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية والتعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	أنشطة التعلمية Shughuli za ujifunzaji	المهارات الخاصة Umahiri mahususi	المهارات العامة Umahiri mkuu
